Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Sita

## Wakati wa Kanisa la Thiatira

Ufunuo 2:18- 29

*"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Thiatira andika; Haya ndiyo anenayo Mwana wa Mungu, Yeye aliye na macho Yake kama mwali wa moto, na miguu Yake mfano wa Shaba iliyosuguliwa sana.*

*Nayajua matendo yako na upendo na imani na huduma na subira yako; tena kwamba matendo yako ya mwisho yamezidi yale ya kwanza.*

*Lakini nina neno juu yako, ya kwamba wamridhia yule mwanamke Yezebeli, yeye ajiitaye nabii na kuwafundisha watumishi wangu na kuwapoteza, ili wazini na kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu.*

*Nami nimempa muda ili atubu, wala hataki kuutubia uzinzi wake.*

*Tazama, nitamtupa juu ya kitanda, na hao wazinio pamoja naye, wapate dhiki kubwa wasipotubia matendo yao;*

*Nami nitawaua watoto wake kwa mauti. Na makanisa yote watajua ya kuwa Mimi ndiye achunguzaye viuno na mioyo. Nami nitampa kila mmoja wenu kwa kadiri ya matendo yake.*

*Lakini nawaambia ninyi na wengine mlioko Thiatira, wo wote wasio na mafundisho hayo, na wasiozijua fumbo za Shetani, kama vile wasemavyo, Sitaweka juu yenu mzigo mwingine.*

*Ila mlicho nacho kishikeni sana, hata nitakapokuja.*

*Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo Yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa,*

*Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, kama vyombo vya mfinyanzi vipondwavyo, kama Mimi Nami nilivyopokea kwa Baba Yangu.*

*Nami nitampa ile nyota ya asubuhi.*

*Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."*

**THIATIRA**

Kihistoria, mji wa Thiatira ulikuwa ndio mdogo wa yote kwa umashuhuri kati ya miji yote ile saba ya Ufunuo. Ulijengwa ndani ya mipaka ya Misia na Ionia. Ulizungukwa na mito mingi, lakini ilijaa wadudu wafyonza damu. Sifa yake moja uliosifika nayo sana ilikuwa kwamba ulijiweza kifedha kwa sababu ya vyama vya ushirika wa biashara ya wafinyanzi, watengenezaji ngozi, wafumaji, mafundi rangi, mafundi wa nguo, nk. Ni katika mji huu ambamo Lidia, yule mwenye kuuza rangi ya zambarau, alitoka. Yeye alikuwa Mzungu mwongofu wa kwanza wa Paulo.

Sasa sababu iliyomfanya Roho kuuchagua mji huu kama tayari uliokwisha kuwa na mambo ya kiroho kwa ajili ya wakati wa nne ilikuwa ni kwa sababu ya dini yake. Dini kuu ya Thiatira ilikuwa ni ibada ya kumwabudu Apolo Tirimnaio ambayo iliunganishwa na madhehebu ya kumwabudu mfalme. Apolo alikuwa mungu jua, na wa pili katika mamlaka kutoka kwa baba yake, Zeu. Alijulikana kama 'kinga ya uovu'; yeye alikuwa mkuu wa sheria za kidini na sadaka (njia ya upatanisho, akilipia makosa ama hatia). Plato alisema juu yake, "Yeye huwaelezea watu kawaida za hekalu, dhabihu na huduma kwa miungu, mbali na desturi zinazohusika na mauti na maisha ya baadaye." Yeye alishirikisha maarifa yake ya 'siku za usoni' na 'mapenzi ya babaye' kwa watu kwa kupitia manabii na maaguzi. Hapo Thiatira ibada hii iliendeshwa na nabii wa kike aliyekalia kiti cha miguu mitatu na kuleta jumbe akiwa kwenye usingizi mzito huku anaona njozi.

Uwezo wa dini hii ulikuwa wa ajabu. Nguvu zake nyingi za hatari mno hazikuwa tu katika milki ya mafumbo, lakini zilikuwa katika kweli kwamba hakuna mtu angaliweza kuwa mwanachama wa vyama hivyo vya ushirika wa kibiashara vilivyowapa watu riziki zao isipokuwa wawe wafuasi wa ibada za hekalu la Apolo. Ye yote aliyekataa kujiunga na karamu hizo za kuabudu sanamu na uasherati alikataliwa kujiunga na vyama hivi vya karne ya kwanza. Ili kuwa sehemu ya maisha ya watu wengine na sehemu ya maisha ya biashara mtu alipaswa kuwa mpagani anayeabudu sanamu.

Ni jambo linalostahili kuangaliwa sana ya kwamba jina lenyewe Thiatira linamaanisha, "Mtawala

Mwanamke." Hivyo basi wakati huu unaainishwa na nguvu itawalayo, nguvu ambayo huwavamia wote kwa ukatili, inawatiisha wote na kutawala kwa udhalimu. Sasa mtawala mwanamke ni laana kubwa kuliko zote duniani. Mtu mwenye hekima kuliko wote ambaye ulimwengu ulipata kumwona alikuwa Sulemani, naye alisema,

*"Moyo wangu ulikazwa katika kujua na kupeleleza, na kuitafuta hekima, na maana ya mambo yaliyoko; ili nifahamu ya kuwa uovu ni upumbavu, na upumbavu ni wazimu.*

*Nami nimeona LILILO NA UCHUNGU KUPITA MAUTI; yaani, MWANAMKE ambaye moyo wake ni mitego na tanzi, na mikono yake ni kama vifungo; yeye ampendezaye Mungu atamponyoka, bali MWENYE DHAMBI atanaswa na yeye.*

*Tazama, asema Mhubiri, mimi nimeyaona hayo kwa kulinganisha hili na hili, ili kuitafuta jumla;*

*Ambayo bado nafsi yangu nikali nikiitafuta, nisiione; mwanamume mmoja katika elfu nimemwona; bali mwanamke mmoja miongoni mwa wote mimi sikumwona."*

Mhubiri 7:25-28.

Paulo alisema,

*"Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala KUMTAWALA mwanamume."*

Tangu Bustani ya Edeni na kuendelea, mwanamke amejaribu daima na akafaulu kuchukua mamlaka juu ya mwanamume, na leo hii ni ulimwengu wa mwanamke na mungu wa kike wa Marekani akiwa ni mwanamke aliye uchi. Kama vile sanamu inayoabudiwa ya mwanamke inayoshuka kutoka angani (kumbuka mikono yake ilikuwa ya fito za chuma) ilionyesha tabia ya ule wa kwanza ama Wakati wa Efeso, vivyo hivyo nguvu zake zimeongezeka mpaka amepata mamlaka kamili, mamlaka ya namna hiyo yakinyakuliwa na tabia yake ya chuma.

Sasa mwanamke hajakusudiwa kuwa na tabia ya chuma. Yeye ni, kulingana na Maandiko Matakatifu, anapaswa kumtii mwanamume. Hilo limeamriwa kwake. Mwanamke ambaye kweli ni mwanamke, mwanamke kabisa kabisa, atakuwa na tabia hiyo. Si jamvi la mlangoni. Hakuna mwanamume halisi anayemfanya mwanamke jamvi la mlangoni. Lakini atapenda kuwa chini ya mamlaka na kutokumtawala mwanamume, kwa maana yeye ndiye kiongozi wa nyumba. Kama akivunja mfano huo ambao amewekewa na Mungu, yeye amepotoka. Mwanamume ye yote anayemruhusu mwanamke achukue mamlaka naye pia amevunja mfano huo na Yeye amepotoka. Hiyo ndiyo sababu mwanamke HAWEZI KUVAA MAVAZI YAMPASAYO MWANAMUME AMA KUKATA NYWELE ZAKE. Hapaswi kamwe kuvaa mavazi yanayompasa mwanamume wala kukata nywele zake. Wakati anapofanya hivyo anaingilia mamlaka ya mwanamume akitwaa mamlaka na kujipotosha mwenyewe. Na mwanamke anapoivamia mimbara jambo ambalo AMEAMRIWA ASIFANYE, anaonyesha yeye ni wa roho ya namna gani. Kuwa mtawala mwanamke ni upinga-Kristo na mbegu za Kanisa Katoliki la Kirumi zimo ndani yake ingawa anaweza kukanusha jambo hili kwa ukali sana. Lakini INAPOFIKIA KWENYE NENO, Neno la Mungu liwe kweli na kila neno la mwanadamu liwe uongo. Amina.

Hebu na turudi nyuma mwanzoni. Katika maumbile ya kawaida ya awali kama tunavyoyajua jambo hilo leo, Mungu alifanya kila kitu katika pea, cha kiume na cha kike. Kulikuweko na kuku wawili—jogoo na kuku jike. Kulikuweko na ng'ombe wawili, ng'ombe jike na fahali. Na vivyo hivyo na kuendelea. Lakini ilipofikia kwa mwanadamu, kulikuweko na mmoja tu. Hawakuwa jozi. Adamu alikuwa ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Alikuwa mwana wa Mungu. Kama mwana wa Mungu asingeweza kujaribiwa na kuanguka. Hilo lisingewezekana. Kwa hiyo Mungu alichukua kitu kilichotokana na mwanamume kusababisha kule kuanguka. Mwanamke hakutoka moja kwa moja kutoka katika mkono wa Mungu kama kiumbe cha kweli cha Mungu. Yeye alitolewa kutoka kwa mwanamume. Na wakati Mungu alipomfanya atolewe kutoka kwa mwanamume alikuwa tofauti sana na majike mengine aliyoyaumba Yeye. Aliweza kumtongozwa. Hakuna jike jingine katika uumbaji linaloweza kuwa zinifu; lakini jike la mwanadamu linaweza kuguswa karibu wakati wo wote.

Na udhaifu huo ndani mwake ulimruhusu Shetani kumtongoza kwa njia ya yule nyoka, na tendo hilo limemleta mwanamke mahali pa kipekee sana mbele za Mungu na Neno Lake. Yeye ni mfano wa mambo yote ya kishenzi, machafu na ya kuchukiza kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine yeye ni mfano wa mambo yote yaliyo safi na mazuri, na matakatifu kama chombo cha Roho na baraka za Mungu. Kwa upande mmoja yeye anaitwa kahaba ambaye amelewa kwa mvinyo ya uasherati wake. Kwa upande mwingine anaitwa Bibi-arusi wa Kristo. Kwa upande mmoja anaitwa Babeli ya Siri, chukizo mbele za Mungu; na kwa upande mwingine anaitwa Yerusalemu Mpya, mama yetu. Kwa upande mmoja yeye ni mchafu sana na mwovu sana na mzinifu sana hata anatupwa bila mjadala katika ziwa la moto kama mahali pekee panapompasa; na kwa upande mwingine anakwezwa mbinguni, akishiriki kiti kile kile cha Mungu kama mahali pekee panapomstahili malkia kama huyo.

Na katika wakati huu wa Kanisa la Thiatira yeye ni MTAWALA MWANAMKE. Yeye ni Babeli ya Siri. Yeye ndiye kahaba mkuu. Yeye ni Yezebeli nabii mke wa uongo. KWA NINI? Kwa sababu mwanamke halisi humtii Mungu. Kristo ndiye kichwa chake. Hana neno ila Lake, hana mawazo ila Yake, hana uongozi ila Wake. Lakini vipi kuhusu kanisa hili? Limelitupa Neno nje, likaziangamiza Biblia na maandishi yenye maana ya wacha Mungu. Limewaua wale ambao wangehubiri kweli. Limewateka wafalme, watawala na mataifa_ anayaongoza majeshi na kusisitiza ya kwamba lenyewe ndilo mwili wa kweli wa Kristo na ya kwamba mapapa wake ndio mahalifa wa Kristo. Limepotoshwa kabisa na ibilisi mpaka lenyewe nalo limekuwa potoshaji la wengine. Ni bibi-arusi wa Shetani na limezaa watoto wake wa dini haramu.

Limetawala wakati wote katika zile Zama za Giza. Kwa zaidi ya miaka mia tisa aliteka nyara na kuangamiza. Liliangamiza sanaa, likaangamiza sayansi, halikuleta kitu cho chote ila mauti mpaka nuru ya ile Kweli ilikuwa karibu imekwisha kabisa na ni sehemu ndogo sana ya nuru iliyosalia. Mafuta na divai vilikuwa karibu kuacha kumiminika; lakini ingawa lilitawala falme za dunia na kudai kwamba watu wote watafute uraia kwake, kulikuweko na kundi dogo lililokuwa la Mungu na uraia wake ulikuwa mbinguni, na hao yeye hakuweza kuwaangamiza. Mungu alilihifadhi kundi Lake dogo; hawangeweza kuangamizwa. Kanisa hili la Rumi lilikuwa ni la kipagani na katili kama Malkia Athalia aliyejaribu kuuangamiza mzao wote wa kifalme na karibu afanikiwe, bali MUNGU ALIMHIFADHI MMOJA, na kutoka kwake huyo wakaja wengine wa wale walio waaminifu. Kwa hiyo Mungu alihifadhi kundi fulani dogo katika usiku huo mrefu wa giza nene na kutokana na kweli yao hatimaye akatokea Luther.

Mtu ye yote anayejua jambo lo lote kuhusu Kanisa Katoliki la Kirumi na kawaida yake ya ibada anaweza kujua kwa nini mji huu wa Thiatira lilichaguliwa na Roho kuwakilisha kanisa katika zile Zama za Giza. Hilo hapo, moja kwa moja mbele ya macho yetu.

## WAKATI WENYEWE

Wakati wa Thiatira ulidumu muda mrefu kuliko nyakati zote, kama miaka 900, tangu mwaka wa 606 hadi 1520.

## MJUMBE

Kanisa lilikuwa limegawanyika tangu siku nyingi katika vikundi viwili, cha Magharibi na cha Mashariki. Mara kwa mara mtengenezaji angeinuka ama katika kimojawapo cha vikundi hivyo ama katika vikundi vyote viwili na kuongoza sehemu fulani ya kanisa kwa muda kidogo kuingia katika uhusiano wa ndani zaidi na Mungu. Mtu kama huyo huko Magharibi alikuwa Fransisi wa Asisi. Akiwa amefanikiwa kwa kweli kwa muda, kazi yake hatimaye iliwekwa chini ya serikali ya dini ya Rumi. Petro Waldo wa Lioni, mfanyi biashara aliyeyakana maisha yake ya kidunia, alikuwa na bidii sana katika kumtumikia Bwana na wengi aliwavuta Kwake; lakini alizuiwa katika kazi yake na akatengwa kwenye ushirika na papa. Si makundi ya Magharibi au ya Mashariki yaliyokuwa na mtu ndani yao ambaye yamkini angeweza kuwa mjumbe kwa wakati huu ikichunguzwa katika nuru ya Maandiko. Hata hivyo, kulikuweko na watu wawili huko kwenye Visiwa vya Uingereza, ambao huduma zao katika Neno na matendo zingeweza kustahimili thibitisho la ile kweli. Walikuwa ni Mtakatifu Patrick na Mtakatifu Columba. Kura ya kuwa mjumbe ilimwangukia Mt. Kolumba.

Ingawa mjumbe wa Wakati wa Thiatira alikuwa Mt. Kolumba, ninataka kueleza kidogo juu ya maisha ya Mt. Patriki kama mfano kwetu na pia kudhihirisha uongo wa dai la Rumi kwamba ati Mt. Patriki alikuwa ni mtu wake zaidi ya ilivyokuwa naye vile vile Joan wa Ark. Patriki alizaliwa na dada wa Mt. Martini katika mji mdogo wa Bonavern kwenye kingo za Mto Klede.

Siku moja wakati alipokuwa anacheza pwani pamoja na dada zake wawili, maharamia wa baharini walikuja na kuwaiba wote watatu. Huko wale dada, walikoenda, hakuna ajuaye, lakini Patriki (jina lake lilikuwa Sukati) aliuzwa kwa sultani fulani huko Ireland ya Kaskazini. Kazi yake ilikuwa ni kuwachunga nguruwe. Ili afanye jambo hili alifundisha mbwa. Mbwa wake walikuwa wamefundishwa vizuri sana hivi kwamba watu wengi walikuja kutoka mbali na karibu kuwanunua. Katika upweke wake alimgeukia Mungu na akaokolewa.

Ndipo ikaja shauku ya kumshurutisha atoroke na kurudi nyumbani kwa wazazi wake. Akabuni mpango uliotumia vizuri sana ustadi wake kama mfugaji. Aliwafundisha mbwa kumlalia na kuufunika mwili wake kwa uangalifu na kutosogea mpaka waamriwe. Ikawa siku moja wakati tajiri wake alipouza mbwa wengi, Patriki aliwapa amri hao mbwa, isipokuwa kiongozi wa hilo kundi, kuingia chomboni. Huyo kiongozi wa kundi hilo ambaye yeye baadaye alimpa ishara ya kisiri alikimbia mbio akakataa kuingia chomboni. Wakati tajiri na huyo mnunuzi walipokuwa wakijaribu kumpata huyo mbwa, Patriki aliingia chomboni na kuwaashiria wale mbwa wamfunike. Ndipo kwa mlio wa filimbi akamleta yule kiongozi wa hilo kundi chomboni na akamlalia. Kwa kuwa Patriki hakuonekana po pote huyo mnunuzi alitweka tanga akaendelea na safari baharini.

Baada ya kuhakikisha ya kwamba nahodha alikuwa amesafiri mbali sana naye hatarudi, Patriki aliwapa hao mbwa ishara nyingine ambayo iliwafanya wafanye ghasia. Ndipo akajitokeza akamwambia nahodha

ya kwamba asipomshusha pwani ya nyumbani kwao angewaamuru mbwa waendelee kufanya ghasia, naye angekiteka hicho chombo.

Hata hivyo, nahodha alikuwa Mkristo, na aliposikia hadithi ya mvulana huyo kwa furaha akamweka ufukoni nyumbani kwake. Huko Patriki akaenda kwenye shule ya Biblia kisha akarudi Ireland ambako kwa Neno na nguvu za Mungu katika ishara nyingi na maajabu aliwavuta maelfu kwa Bwana. Na hakuna wakati wo wote yeye aliwahi kwenda Rumi wala hakuna hata wakati mmoja alipotumwa na Rumi. Ukweli wa mambo ni kwamba wakati Rumi hatimaye ilipopata mamlaka katika kisiwa hicho na walipoona wakati ulikuwa unafaa, waliua Wakristo zaidi ya 100,000 ambao kwa miaka mingi walikuwa wamechipuka kutoka kwenye lile kundi la kwanza lililomjia Bwana chini ya Mt. Patriki.

Yapata miaka 60 baada ya kifo cha Mt. Patriki, Columba alizaliwa katika Mkoa wa Donegali, Ireland ya Kaskazini, kwa jamaa ya kifalme ya Fergusi. Yeye akawa mwanazuoni mwenye akili nyingi, aliyejitenga kwa Bwana, akikariri karibu Maandiko yote. Mungu alimwita kwa sauti iliyosikika wazi awe mmishenari. Baada ya yeye kusikia sauti ya Mungu, hakuna kitu kiliweza kumzuia, na huduma yake ya kimiujiza imewafanya wanahistoria wengi kumsifu sana kwamba yeye ndiye hasa anayewafuatia mitume. Huduma yake ilikuwa kuu sana huku ikifuatwa na ishara za kimiujiza hata baadhi (zaidi sana wanafunzi huko Rumi) wamefikiria taarifa hizo zilitiwa chumvi.

Katika moja ya safari zake za kimishenari, alipokuwa anaukaribia mji uliozingirwa kote na ukuta, alikuta amefungiwa malango. Akainua sauti yake katika maombi kwamba Mungu aweze kuingilia kati na kumruhusu apate njia ya kuwafikia watu awahubirie. Lakini hapo alipokuwa anaomba wachawi wa nyumba ya mfalme walianza kumsumbua kwa sauti kuu za kelele. Kisha akaanza kuimba zaburi. Alipokuwa anaimba, Mungu aliikuza sauti yake sana hata akayafunika yale makelele ya wale makafiri. Mara yale malango yakafunguka yenyewe. Yeye aliingia na kuhubiri Injili, akiwavuta wengi kwa Bwana.

Wakati mwingine ambapo alikuwa amefungiwa tena nje ya kijiji fulani, wakati alipogeuka kurudi, mwana wa sultani ghafla akawa mgonjwa mahututi, karibu ya kufa. Mt. Columba alitafutwa upesi akaitwa arudi. Alipoomba maombi ya imani mvulana huyo aliponywa mara moja. Kijiji hicho kikafunguka basi kwa kuhubiriwa kwa Injili.

Injili isiyoghoshiwa iliyohubiriwa na Columba na wahudumu wenzake ilienea Skotland nzima, ikaigeuza kumwelekea Mungu. Pia ilifurika ikaingia Ireland na Ulaya ya Kaskazini. Njia yake ya kueneza Injili ni ile ambapo labda watu kumi na wawili chini ya kiongozi mmoja wangeingia katika eneo moja jipya na kujenga mji halisi wa makao makuu ya Injili. Miongoni mwa watu hawa kumi na wawili wangekuwemo maseremala, waalimu, wahubiri, nk., wote wakiwa wamefundishwa Neno vizuri sana pamoja na kuishi maisha matakatifu. Koloni hili dogo lilikuwa limezungushiwa ukuta. Muda si muda eneo hili lingezungukwa na wanafunzi na jamaa zao katika nyumba zao wenyewe, wakijifunza Neno na kujitayarisha kutoka waende wakamtumikie Bwana kama wamishenari, viongozi, na wahubiri. Hao wanaume walikuwa huru kuoa ingawa wengi hawakuoa, kusudi wamtumikie Mungu vizuri zaidi. Hawakufungwa na msaada wa serikali, na kwa kufanya hivyo wakazikwepa siasa. Badala ya wao kushambulia dini nyingine waliifundisha ile kweli kwa kuwa waliamini ya kwamba ile kweli ilikuwa ni silaha ya kutosha kutimiza kusudi alilokuwa nalo Mungu kwa ajili yao. Walikuwa huru kabisa na Rumi.

Mt. Columba alikuwa mwanzilishi wa shule kubwa ya Biblia kwenye kisiwa cha Hai (mbele ya pwani ya Kus. Magh. mwa Skotland). Wakati alipokwenda huko hicho kisiwa kilikuwa kame sana na chenye miamba sana hata hakingeweza kuzaa chakula cha kutosha kwa ajili yao wote. Lakini Columba alipanda mbegu kwa mkono mmoja huku akiinua huo mkono mwingine juu katika maombi. Leo kisiwa hicho ni kimoja cha visiwa vyenye rutuba sana duniani. Kutoka kwenye kisiwa hiki cha makao makuu ya Biblia kukatoka wanachuoni hodari waliokirimiwa hekima na nguvu za Mungu.

Wakati nilipoisoma historia ya mtumishi huyu mashuhuri wa Mungu na kazi za ajabu alizotenda, moyo wangu ulihuzunika kuona kwamba ngvuvu za kipapa, zikitamani kuwaleta watu wote kwenye mikono yake, zilikuja na hatimaye zikachafua maeneo haya ya kimishenari na kuangamiza ule ukweli kama ulivyofundishwa na Columba.

**SALAMU**

Ufunuo 2:18,

> *"Haya ndiyo anenayo Mwana wa Mungu, Yeye Aliye na macho Yake kama mwali wa moto, na miguu Yake mfano wa shaba iliyosuguliwa sana."*

Ufunuo wa Uungu kwa Wakati wa Thiatira ni kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Wakati mmoja alipokuwa katika siku Zake za mwili Yeye alijulikana kama Mwana wa Adamu. Lakini sisi tangu sasa hatumjui Yeye tena kwa jinsi ya mwili. Yeye si Mwana wa Adamu tena, yule Nabii Mkuu, Ambaye katika Yeye Mwenyewe alikusanya pamoja nabii zote. Mwana wa Pekee amerudi katika kifua cha Baba. Sasa tunamjua kwa jinsi ya nguvu za kufufuka. Yeye amefufuka na amejitwalia Mwenyewe nguvu Zake kuu

Naye ni zaidi ya yote na juu ya yote kwa sifa za utukufu Wake. Hatashiriki utukufu Wake na mtu mwingine. Hatampa mtu ye yote uongozi Wake juu ya kanisa.

Yeye anauangalia Thiatira, na hapa anaona katika mji huo na katika wakati ule wa nne heshima ambayo ni Yake peke Yake, imepewa mwingine. Macho Yake yanawaka kwa moto wa hasira na hukumu anapomwona Apolo akiheshimiwa kama Mwana wa Mungu, wakati Yeye peke Yake ndiye Mwana wa Pekee wa Baba. Jinsi hukumu Yake inavyopaswa kuwa mbaya juu ya dini hii ya Wakati wa Thiatira ambapo wafuasi wa kanisa kama vile wapagani wanaomwabudu mwana wa mungu (Apolo mwana wa Zeu), wanavyomwinua mtawala wa kibinadamu na kumsujudu, wakiungwa mkono na nguvu za serikali. Kwa kuwa hivyo ndivyo alivyoona hasa. Kanisa Katoliki la Kirumi, likiwa limezama kabisa katika ibada za sanamu zenye msingi wake kwenye ibada za mungu jua (Apolo) lilikuwa limemwinua mtu fulani kuwa mungu halisi (papa) kwa muungano wa kanisa na serikali. Kwa kuwa Tomaso Akwinasi na Alverusi Pelagiusi walieleza na kusema ya kwamba: "Papa anaonekana kwa hao wanaomwangalia kwa jicho la kiroho, kuwa, si mwanadamu bali ni Mungu fulani. Hakuna mipaka kwa mamlaka yake. Hakuna mipaka katika mamlaka yake. Anaweza kutangaza lo lote atakalo kuwa ni kweli na anaweza kuwanyang'anya watu wo wote haki zao apendavyo. Kutilia shaka nguvu hizi zilizoenea kote duniani kutaleta kufungiwa nje ya wokovu. Adui wakuu wa kanisa ni wale wazushi wa dini ambao hawatavaa nira ya utiifu wa kweli.

*"Kuna mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, mwanadamu Kristo Yesu (Mwana wa Mungu.)"*

I Timotheo 2:5.

Lakini papa wa Rumi amelibadilisha Neno. Yeye alilifanya, "mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu (si wanadamu)". Kwa hiyo sasa yeye anapatanisha kati ya mpatanishi na wanadamu. Lakini hakuna mpatanishi mwingine ila Mwana. Papa hutangaza wokovu kupitia kwa kanisa la Rumi. Lakini hakuna wokovu ila kwa kupitia kwa Mwana wa Mungu. Si ajabu hayo macho yanawaka katika hukumu ya hasira kali. Si ajabu hiyo miguu ni kama shaba iliyosuguliwa sana anaposimama akiwa tayari kuzikanyaga-kanyaga zikawa unga na vumbi falme hizi potovu za ulimwengu huu. Mungu ashukuriwe kwa miguu hiyo yenye nguvu ya shaba. Imepitia katika hukumu kwa ajili yetu. Sasa hiyo ndiyo msingi wetu kwa maana aliyoyapata ni yetu. Tunasimama tumetambulishwa katika Yeye, Yesu Mwana wa Mungu.

Ilikuwa ni katika wakati huu ambapo tunashuhudia kuinuka kwa Uislamu ambao ulimkana Mwana wa Mungu na kutangaza kifo kwa wale wote waliojiita Wakristo.

Ilikuwa pia ni katika wakati huu ambapo kanisa la uongo liliasi amri ya kwanza ya Mwenyezi Mungu na likaingilia upesi kuivunja amri ya pili kwa maana lilimweka papa wake katika mahali pa Yesu Kristo na kuanzisha na kulazimisha ibada za sanamu sana hivi kwamba ilimaanisha kifo kwa wale waliokataa hizo sanamu kuwekwa ndani ya kanisa. Chini ya Malkia Theodora, peke yake, tangu mwaka wa 842 hadi 867 zaidi ya watakatifu 100,000 waliuawa kwa sababu walihesabu kwamba sanamu hazina thamani yo yote.

Hakika wakati huu hauna budi kutubu ama utapoteza yote. Huyo hapo amesimama Bwana wa utukufu, Mungu aliye Mungu kabisa_Neno Lake limewekwa kando, utu Wake umekataliwa, lakini mikono ya binadamu na mioyo ya mwanadamu haiwezi kumwondoa mamlakani. Acha wamkane, Yeye anadumu mwaminifu. "Msiogope enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme. Na wakati nitakapokuja kwa miguu ya shaba na macho yanayowaka moto nitalipa; hukumu ni yangu, nitawajazi," asema Bwana.

**SIFA**

Ufunuo 2:19,

> *"Nayajua matendo yako na upendo na imani na huduma na subira yako na matendo yako; na tena kwamba matendo yako ya mwisho yamezidi yale ya kwanza."*

Hapa tena tunaona matamshi yale yale ya utangulizi, "Nayajua matendo yako." Mwana wa Mungu, Mwenyewe, alisema, "Mnisadiki Mimi kwa ajili ya kazi zenyewe." Yeye alitilia mkazo kazi Zake mwenyewe wakati alipokuwa duniani. Kazi alizofanya zilikuwa zimeamriwa na Mungu kuvuvia imani katika Yeye. Ilikuwa ni sehemu kubwa ya huduma Yake.

Roho Wake Mtakatifu katika mtume Paulo alisema,

> *"Maana tu kazi Yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.."*

Waefeso 2:10.

*Kazi hizi zilikuwa zihuishe imani katika Yeye kwa maana zingeonyesha uhusiano huo Kwake ambao Paulo alieleza kama "tuliumbwa katika Yeye."*

Sasa kazi kamwe hazitapachukua mahali pa imani katika Mungu kwa ajili ya wokovu wetu. Lakini kazi zitaonyesha imani yetu ambayo tayari imewekwa ndani Yake. Matendo mema hayatakuokoa, lakini yatatokea kutoka katika maisha yaliyookolewa kama tunda kwa Bwana. Ninaamini katika matendo mema. Hata kama mtu hajaokolewa, anapaswa kufanya matendo mema na ajitahidi awezavyo. Jambo la kuchukiza mbele za Mungu ni kwa wanadamu kufanya matendo mabaya na halafu waseme wanatenda mapenzi ya Bwana. Hivyo ndivyo maaskofu na mapapa na serikali ya dini ya Rumi walivyokuwa wanafanya. Walikuwa wanaua, wakiharibu, na kufanya kila namna ya uovu katika Jina la Bwana. Waliishi maisha kinyume kabisa na yale yanayofundishwa na Neno. Katika siku hiyo ya uovu hao waamini wa kweli waling'aa kama nuru gizani walipokuwa wanaendelea kutenda mema; kwa kuwa walirudisha baraka kwa laana, nao wakatekeleza ile kweli kumheshimu Mungu hata ingawa wengi walikufa kwa ajili hiyo.

Katika aya hii Yeye anawasifu watoto Wake kwa sababu walikuwa wanaishi maisha yaliyobadilishwa. Kazi zao zilishuhudia Roho mpya aliyekuwa ndani. Watu waliona matendo yao mema na kumtukuza Mungu. Naam bwana, kama wewe ni Mkristo utafanya yaliyo mema. Kazi zako zitaonesha ya kwamba moyo wako uko sawa. Na haitakuwa ni jambo ambalo unaigiza, kwa maana utafanya mapenzi Yake hata Yake wakati hakuna mtu anayekuona ila Mungu, na utafanya mapenzi Yake hata kama itakugharimu maisha yako.

*"Najua upendo wako, na imani, na huduma na subira yako."* Utaona ya kwamba upendo wao umewekwa katikati ya 'matendo' na 'huduma'* Na hapo ndipo mahali pake panapofaa, kwa maana bila upendo kazi zetu hazikubaliki mbele za Mungu na wala huduma zetu. Paulo akizungumza na Wakorintho alisema, "Bila upendo, si kitu mimi, na lo lote nifanyalo halina faida isipokuwa linafanywa katika upendo." Sasa unaweza kuona papa hapa ya kwamba waamini hawa hawakuwa katika tabaka lile la Wanikolai waliotenda kazi kama njia ya wokovu ama ya kupendwa na watu. Walifanya kazi zao kutokana na pendo la Mungu lililokwisha kumiminwa katika mioyo yao na Roho Mtakatifu. Pendo hilo mioyoni mwao lilikuwa pendo la Mungu kwa ajili ya walio Wake. Yesu alisema, "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi WANGU, kwamba mna upendo ninyi kwa ninyi." Wapagani walioyaona maisha ya Wakristo wa mwanzoni walisema, "Tazama jinsi wanavyopendana." Yohana alisema

> *"Kila apendaye amezaliwa na Mungu."*

I Yohana 4:7.

Ninataka kutoa onyo papa hapa. Inanenwa kuhusu siku za mwisho ya kwamba kwa sababu ya kuongezeka maasi upendo wa wengi utapoa. Katika Laodikia, ama wakati wa mwisho, kujipenda, na kupenda mali kutachukua mahali pa pendo la kweli la Mungu. Tunapaswa kujikinga na nguvu za dhambi katika siku hizi za mwisho. Watu wengi sana wanakuwa wagumu sana kwa sababu hawajatambua nguvu za roho hii ya siku ya mwisho. Wakati umewadia wa kumkaribia Mungu na kumruhusu ayajaze maisha yetu na upendo Wake, la sivyo tutasikia ubaridi wa kanisa la siku za mwisho, na kuikataa kweli ya Mungu ambayo ndiyo pekee inayoweza kutusaidia.

Katika miaka hiyo ya giza na ya kutisha mzabibu wa kweli ulishikilia upendo wake kwa Mungu na upendo wa ndugu. Mungu aliwasifu kwa ajili ya jambo hilo.

*"Naijua huduma yako."* Yesu alisema, "Yeye aliye mkubwa wenu ndiye mtumishi wa wote." Mtu mwenye hekima alitoa matamshi yake juu ya msemo huo. Hivi ndivyo alivyosema, "Historia pekee ndiyo itakayothibitisha ukweli wa msemo huo." Mtu huyo alikuwa sahihi. Watu wote walio wakuu kweli wa historia wamekuwa watumishi. Hao waliodai kutumikiwa; hao waliowatesa watu; hao waliotafuta sikuzote kuwa wakubwa, wameishia katika aibu. Hata walio matajiri sana wamehukumiwa na Mungu wakati hawakutumia mali yao vizuri. Lakini angalia katika historia na utaona ya kwamba wale waliokuwa wakuu kweli walikuwa ni wale waliowatumikia wengine. Historia haiwezi kamwe kuwasifu wale ambao walitendewa mengi, lakini daima itawasifu wale waliowafanyia mengi wengine.

Sasa hebu na tutumie jambo hilo kwetu. Hata kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, vivyo hivyo sisi nasi tunapaswa kufuata mfano huo. Mwangalie anapoinama kwenye miguu ya wale mitume na kuitawadha miguu yao iliyochoka na michafu. Yeye alisema, "Hamjui sasa nifanyalo, lakini mtafahamu baadaye. Lakini mnaloniona Mimi nikifanya, mnapaswa kulifanya pia." Yeye alifanyika mtumishi kusudi Mungu aweze kumwinua juu kuliko vitu vyote. Na siku moja katika hukumu ya watakatifu tutamsikia Yeye akisema, *"Vema, MTUMWA mwema na mwaminifu, ingia katika furaha ya Bwana."* Ni vigumu kuwa mtumishi daima. Lakini wale wanaotumika na kutaabikia wengine siku moja wataketi pamoja Naye katika kiti Chake cha enzi. Litakuwa jambo la thamani kuliko yote, wakati huo. "Na tumtumikie Bwana, tangu mapambazuko hata machweo ya jua, Na tuzungumze kuhusu upendo Wake wote wa ajabu na huruma Zake, Na hapo maisha yote yatakapokwisha na kazi zetu duniani zimekwisha, Na majina yaitwapo kule juu nitakuweko."

*"Naijua imani yako."* Sasa Yeye hasemi hapa kama alivyoliambia kanisa huko Pergamo, "unaishika imani YANGU." Yeye haneni kuhusu imani Yake sasa, lakini anawasifu kwa ajili ya uaminifu wao. Na anapofanya jambo hilo anataja pia 'subira' yao. Sasa uaminifu na saburi vinaambatana.

Kwa kweli subira ni matokeo ya uaminifu, kwa maana Yak. 1:3 inasema,

*"Kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi."*

Hakuna kwa vyote vyote njia nyingine ya kupata subira. Haina budi kuja kwa kujaribiwa kwa imani yetu.

Warumi 5:3,

*"Dhiki kazi yake ni kuleta saburi."*

Jinsi Mungu anavyothamini sana kuimarishwa kwa subira yetu inaonekana katika Yak. 1:4,

*"Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno."*

Mapenzi ya Mungu kwetu ni Ukamilifu. Na huo ukamilifu ni subira—kumngojea Mungu na kumngoja Mungu. Hii ndiyo njia ya kuumba tabia. Jinsi Mungu alivyowasifu sana watakatifu hawa wa zile Zama za Giza. Wenye saburi kama ya wanakondoo wakiongozwa machinjioni, walimtumikia Mungu kwa upendo, uaminifu. Hayo tu ndiyo waliyotaka maishani, kumtumikia tu Bwana wao. Jinsi thawabu yao itakavyokuwa kubwa.

*"Nayajua matendo yako; tena kwamba matendo yako ya mwisho yamezidi yale ya kwanza."*

Hili bila shaka lina maana sana. Wakati giza la wakati huo lilipoongezeka; wakati orodha ya heshima ya wafia imani ilipozidi kuwa ndefu siku kwa siku, walifanya kazi kwa juhudi zaidi, walitumika zaidi, na imani yao ikaongezeka. Iikuwa ni huzuni iliyoje kwamba katika Wakati wa Efeso upendo ulififia. Na kweli hakuna kitu kilichosemwa juu ya kuongezeka kwa taabu ya upendo katika zile nyakati nyingine; lakini katika wakati huu, katika wakati ulio na giza sana kuliko nyakati nyingine zote, wao walimtumikia hata na zaidi. Ni somo lililoje. Hakuna kukoma kwa huduma hii ya neema ya kumpenda Bwana, lakini zaidi ni kuongezeka kwake. Hiyo ndiyo siri. Hebu adui ajaribu kupinga utumishi wetu kwa Bwana_jibu letu ni kuongezeka huduma. Wakati waliodhaifu wanapolia kwa hofu, huo ndio wakati wa kupiga makelele ya ushindi.

*"Nayajua matendo yako; tena kwamba matendo yako ya mwisho yamezidi yale ya kwanza."*

Sasa kama vile tulivyokwisha kusema, wakati huu unaitwa Zama za Giza kwa sababu ulikuwa kweli ndio wakati uliokuwa wa giza sana katika historia yote. Ulikuwa wakati wa Papa Inosenti III aliyedai ya kwamba yeye ndiye "aliye badala ya Kristo_mfalme mkuu juu ya kanisa na dunia," aliyeanzisha BARAZA KUU LA KUHUKUMU WAAMINI ambalo chini ya uongozi wake lilimwaga damu nyingi zaidi kuliko katika wakati mwingine wo wote isipokuwa katika wakati wa yale Matengenezo. Ulikuwa ni wakati wa uasherati, utawala wa malaya. Sagarius III alikuwa na malaya wake na "aliijaza kwaya ya papa na hawara na wana wa haramu na kuifanya ikulu ya papa kuwa pango la wanyang'anyi." Anastazia III alikabwa koo mpaka akafa na Marozia ambaye alikuwa kahaba wa Sagarius. Yohana wa XI alikuwa mwana wa haramu wa Marozia. Yohana XII alikuwa mjukuu wa Marozia naye "aliwanajisi wajane na mabikira na aliuawa akiwa kwenye tendo la uzinzi na mume wa huyo mwanamke aliyekuwa ameghadhabika sana." Ulikuwa ni wakati wa Mafarakano ya Kipapa kwa kuwa serikali mbili za mapapa (moja ikitawala kutoka Avignon na hiyo nyingine kutoka Rumi) walilaaniana na kupigana wao kwa wao. Mapapa hawa hawakuwa tu na hatia ya matendo mabaya ya uzinzi (wakizaa chungu mbovu ya watoto haramu, wakifanya ulawiti nk.) lakini walikuwa na hatia ya kuuza vyeo vya ukuhani kwa wazabuni waliolipa pesa nyingi zaidi.

Mapapa hawa hawakuwa tu na hatia ya matendo mabaya ya uzinzi (wakizaa chungu mbovu ya watoto haramu, wakifanya ulawiti nk.) lakini walikuwa na hatia ya kuuza vyeo vya ukuhani kwa wazabuni waliolipa pesa nyingi zaidi. Juhudi zao zilikuwa motomoto hivi kwamba hata waliandaa njia kwa ajili ya matengenezo yaliyokuwa yanakuja. Kwa hiyo kama vile Neno linavyosema kuhusu wakati huo, "matendo yako ya mwisho (mwisho wa wakati huo) yamezidi ya kwanza."

Neno, Thiatira, lina maana mbalimbali ambazo kati ya hizo mojawapo ni "Dhabihu ya Daima." Kwa wengi hii inaaminiwa kuwa ni unabii kuhusu matumizi ya Misa ambayo ni kutolewa kwa daima kwa dhabihu ya Kristo. Hilo ni wazo zuri sana, lakini linaweza pia kumaanisha dhabihu ya daima katika maisha na taabu za waamini wa kweli wa Bwana.

Hakika hawa watakatifu wa Thiatira walikuwa ndio malimbuko ya zao, waliojaa Roho Mtakatifu na imani, walioumbwa watende matendo mema, wakionyesha sifa Zake, wakiacha kuthamini maisha yao wenyewe, lakini kwa furaha wakitoa yote waliyo nayo kama dhabihu impendezayo Bwana.

**KEMEO**

Ufunuo 2:20,

*"Lakini nina neno juu yako, maadamu wamridhia (kuchukuana na) yule mwanamke Yezebeli, yeye ajiitaye nabii na kuwafundisha watumishi wangu na kuwapoteza, ili wazini na kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu."*

Sasa mkiwa mmeshikilia aya hii nawataka mshuke chini kwenye aya ya 23 na mwone udhihirisho wa kweli kuu niliyokuwa nikiwaletea wakati huu wote. "Nami nitawaua watoto wake kwa mauti. Na makanisa yote watajua ya kuwa Mimi Ndiye achunguzaye viuno na mioyo." Kila wakati nimekuwa nikisema ya kwamba kwa kweli kuna makanisa mawili, ingawa Roho ananena na yote mawili katika kila wakati, kana kwamba yalikuwa ni moja. Hapa imesemwa dhahiri ya kwamba kuna makanisa, na inaelezea wazi pia kwamba baadhi ya makanisa hayo kwa hakika kabisa HAYAJUI ya kwamba Yeye Ndiye achunguzaye viuno na mioyo. Yeye atawathibitishia ya kwamba ni hilo kweli. Sasa basi, ni makanisa gani yatakuwa wale wasiojua ukweli huu? Bila shaka ni lile kundi la mzabibu wa uongo kwa sababu waamini wa kweli hakika wanajua ya kwamba hukumu huanzia katika nyumba ya Mungu, nao wakiwa wacha Mungu, wanajichunguza wasije wakahukumiwa.

Sasa kwa nini Mungu anayaita makanisa haya ni makanisa Yake hata ingawa wao ni mzabibu wa uongo? Ukweli wa mambo ni kwamba wao ni Wakristo. Lakini wao si Wakristo wa Roho. Wao ni Wakristo wa mwilini. Wao wanalichukua Jina hilo bure. Marko 7:7, "Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu." Lakini kweli wao ni Wakristo kwa kuwa ni kitu gani kingine tena wangeweza kuwa? Mwislamu ni Mwislamu. Hiyo ndiyo dini yake haidhuru anaiishije kwa sababu yeye anakubaliana kwa akili na yale Kurani inayofundisha.

Vivyo hivyo Mkristo ni Mkristo mradi tu yeye anakubaliana na ukweli kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, aliyezaliwa na bikira, alisulibishwa na akafa na akafufuka tena, ya kwamba Yeye ndiye Mwokozi wa wanadamu, na kadhalika. (Kwa kweli katika Wakati wa Laodikia kutakuweko na wale wanaojiita Wakristo kwa sababu ati wanakubaliana na sifa nzuri za Yesu, huku wakijiwekea haki ya kuukana Uungu Wake. Wakristo wa Kisayansi wamefanya jambo hilo tayari pamoja na watu wengi ambao wanahubiri Injili ya kijamii). Yeye ni Mkristo wa jina na ni mfuasi wa kanisa. Lakini yeye si mwamini WA KWELI ama mwamini wa Kiroho. Mwamini wa namna hiyo ni yule ambaye amebatizwa katika mwili wa Kristo na ni mshiriki Wake. Mwamini wa namna hiyo ni yule ambaye amebatizwa katika mwili wa Kristo na ni mshiriki Wake.ngano wala yasing'olewe. Hiyo ni amri ya Mungu. Siku yao ya kufungwa matita-matita na kuchomwa moto inakuja; lakini bado haijaja.

Kwa hiyo Roho ananena na kundi hili lililochanganyikana. Kwa upande mmoja Yeye anasifu, na kwa upande mwingine anakemea. Amesema yaliyo heri kwa mwamini wa kweli. Sasa Yeye anaonya yale ule mzabibu wa uongo unayopaswa kufanya kama utasimama uhesabiwe haki mbele za Bwana.

## YULE MWANAMKE YEZEBELI

Mtume Yakobo alituonyesha njia ambayo dhambi hupitia.

Yakobo 1:14-15,

*"Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa.*

*Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti."*

Sasa hiyo ndiyo picha hasa ya yale yanayotukia katika nyakati za kanisa. Kwa kuwa dhambi haikuanza katika kitu cho chote ila hisia tu, kwa hiyo mauti kwa kanisa ilianza na matendo rahisi, na yasiyotambulikana sana ya Wanikolai. Kutoka matendo yakawa fundisho. Kutoka kwenye fundisho yalizikamata nguvu za serikali na kuingiza upagani. Sasa katika wakati huu linaenda kwa nabii wake mwenyewe (mwalimu) na kwa hiyo linaendelea kusafiri mpaka litakapojikuta kwenye ziwa la moto, kwa maana huko ndiko litakakoishia, katika ile mauti ya pili.

Sasa malalamiko yote ya Mungu dhidi ya wakati huu wa nne yanaonekana katika lawama Zake juu ya nabii huyu wa kike, Yezebeli. Na ili kufahamu ni kwa nini hasa Yeye anamlaumu namna hiyo, itatubidi kuchunguza historia yake katika Biblia na wakati tutakapoona yale aliyofanya kule nyuma, tutajua yale yanayoendelea wakati huu.

Jambo la kwanza na lililo muhimu sana tunalojifunza juu ya Yezebeli ni kwamba yeye SI binti wa Ibrahimu, wala kuingizwa kwake katika makabila ya Israeli hakukuwa kuingizwa kwa kiroho kama kule kuingizwa kwake Ruthu, yule Mmoabi. La bwana. Mwanamke huyu alikuwa binti Wa Ethbaali, mfalme wa Sidoni (I Wafalme 16:31), ambaye alikuwa kuhani wa Astarte. Yeye alinyakua ufalme kwa kumwua Felesi, aliyemtangulia. Kwa hiyo tunaona mara moja ya kwamba yeye alikuwa binti wa mwuaji. (Hii hakika inatukumbusha juu ya Kaini.) Na namna alivyokuwa sehemu ya Israeli si kwa kupitia njia za kiroho ambazo Mungu alikuwa ameamuru kwa ajili ya kuwaingiza Mataifa; lakini aliingia kwa KUOLEWA na Ahabu, mfalme wa yale makabila kumi ya Israeli. Sasa muungano huu kama tulivyoona haukuwa wa Kiroho; ulikuwa wa kisiasa. Na hivyo mwanamke huyu aliyekuwa amezama katika ibada za sanamu hakuwa na shauku hata

kidogo ya kuwa mwabudu wa Mungu Mmoja aliye wa Kweli, bali badala yake alikuja ameyakinia kuwageuza Israeli wamwache Bwana.

Sasa Israeli (yale makabila kumi,) tayari walikuwa wamejua ni nini kuabudu ndama wa dhahabu, bali walikuwa bado hawajajiuza kwa ibada za sanamu, kwa maana Mungu aliabudiwa na torati ya Musa ilikubaliwa. Bali tangu wakati wa Ahabu alipomwoa Yezebeli, ibada za sanamu ziliendelea katika mtindo wa kutisha mno. Ilikuwa ni wakati huu mwanamke huyu alipokuwa kuhani mwanamke katika mahekalu ambayo alimjengea Astarte (Vinasi) na Baali (mungu jua) ambapo Israeli walifikia upeo wa hatari sana katika maisha yao.

Tukiwa tumeshikilia jambo hili moyoni tunaweza sasa kuanza kuona kile ambacho Roho wa Mungu anaelezea katika wakati huu wa Thiatira. Hiki hapa.

Ahabu akamwoa Yezebeli naye alifanya jambo hilo kama werevu wa kisiasa kuimarisha ufalme wake na kuulinda. Hivyo ndivyo kanisa lilivyofanya kabisa wakati lilipoolewa chini ya Konstantino. Wote waliungana kwa sababu za kisiasa, ingawa waliingiza hali ya kiroho ndani yake. Sasa hakuna mtu anayeweza kunifanya nisadiki kwamba Konstantino alikuwa Mkristo. Yeye alikuwa mpagani mwenye yale yaliyoonekana kama mapambo ya Kikristo. Alichora misalaba myeupe kwenye ngao za askari. Alikuwa mwanzilishi wa Mashujaa wa Columba. Aliweka msalaba juu ya mnara uliochongoka wa Mt. Sofia na hapo akaanzisha mapokeo.

Wazo alilokuwa nalo Konstantino lilikuwa kuwaleta watu wote pamoja, wapagani, Wakristo wa jina na Wakristo wa kweli. Na kwa kitambo kidogo ilionekana kana kwamba angefanikiwa kwa maana waamini wa kweli walikuja kuona kama wangeweza kuwarudisha wale waliokuwa wameondoka kwenye Neno. Walipoona ya kwamba hawangeweza kuwarudisha kwenye ile kweli, walilazimika kutengana na hilo shirika la kisiasa. Ndipo walipofanya hivyo, waliitwa wazushi na wakateswa.

Hebu niseme papa hapa ya kwamba tunalo jambo lile lile likiendelea sasa hivi. Watu wote wanaungana pamoja. Wanaandika Biblia ambalo litamfaa kila mmoja iwe ni Myahudi, Mkatoliki, ama Mprotestanti. Wao wana Baraza lao wenyewe la Nikea bali wanaliita Baraza la Ekumeni. Na unajua haya mashirika yote yanawapiga vita akina nani? Yanawapiga vita Wapentekoste wa kweli. Simaanishi shirika linaloitwa Pentekoste. Ninamaanisha wale ambao ni Wapentekoste kwa sababu wamejazwa na Roho Mtakatifu nao wana ishara na karama miongoni mwao kwa maana wao wanatembea katika kweli.

Wakati Ahabu alipomwoa Yezebeli kwa sababu za kisiasa yeye aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Ukijiunga na shirika fulani basi unauza haki yako ya mzaliwa wa kwanza, ndugu, amini usiamini. Kila kundi la Kiprotestanti lililowahi kutoka kisha likarudi huko huko lilikotoka waliuza haki zao za mzaliwa wa kwanza, na unapouza haki yako ya mzaliwa wa kwanza, wewe ni kama tu Esau_unaweza kulia na kutubu utakavyo, bali haitakufaa kitu. Kuna jambo moja tu unaloweza kufanya na hilo ni, "Tokeni kwake, enyi watu wangu, na mwache kuzishiriki dhambi zake!" Sasa kama hudhani ninasema kweli, hebu jibu tu swali hili moja. Kuna mtu ye yote aishiye anayeweza kuniambia ni kanisa gani ama ni tukio gani la Mungu lililopata kuwa na ufufuo na likapata kurudi baada ya kuunda shirika na kufanyika madhehebu? Someni historia zenu. Huwezi kupata moja_hata moja.

Ilikuwa ni saa ya usiku wa manane kwa Israeli wakati walipojiunga na ulimwengu na kuacha ya Kiroho kuendea yale ya kisiasa. Ilikuwa ni saa sita usiku huko Nikea wakati kanisa lilipofanya jambo lile lile. Ni saa sita usiku ambapo makanisa yanakusanyika.

Basi wakati Ahabu alipomwoa Yezebeli alimruhusu kuchukua fedha za serikali na kujenga majumba mawili makubwa sana ya kuabudia ya Astarte na Baali. Lile alilojengewa Baali lilikuwa kubwa vya kutosha kwa Israeli wote kuja na kuabudia hapo. Na wakati Konstantino na kanisa walipofanya arusi yeye alilipatia kanisa majengo, na kutengeneza madhabahu na sanamu, na akaunda serikali ya kanisa ambayo tayari ilikuwa inaumbika.

Wakati Yezebeli alipoungwa mkono na nguvu za serikali aliwalazimisha watu dini yake na akawaua manabii na makuhani wa Mungu. Hali ilikuwa mbaya sana hata Eliya, mjumbe wa siku yake, alifikiria alikuwa ndiye peke yake aliyebakia; bali Mungu alikuwa na wengine 7,000 ambao walikuwa bado hawajampigia magoti Baali. Na sasa hivi kule nje kati ya hayo madhehebu ya Wabatisti, Wamethodisti, Wapresbiteri, nk., kuna baadhi yao watakaotoka na kumrudia Mungu. Nataka mjue mimi sipambani, sasa, na sijawahi kupambana na watu. Ni madhehebu_taratibu ya shirika ambayo ninapambana nayo. Mimi sina budi kuipinga kwa sababu Mungu anaichukia.

Sasa hebu na tusimame kwa dakika moja hapa turudie kuelezea kile tulichoelezea juu ya ibada kule Thiatira. Nilisema ya kwamba wao walimwabudu Apolo, (ambaye alikuwa mungu jua) pamoja na mfalme. Sasa huyu Apolo aliitwa 'mkinga maovu.' Aliwakingia watu maovu. Aliwabariki na alikuwa mungu halisi kwao. Alipaswa kuwafundisha watu. Alielezea habari za ibada, na taratibu za hekalu, ibada kwa miungu, juu ya kutoa dhabihu na kuhusu mauti na uzima baada ya kufa. Jinsi alivyotenda haya ilikuwa ni kwa kupitia kwa nabii wa kike aliyeketi amelala fofofo juu ya kiti cha miguu mitatu. Jamani! Mnaona jambo

hilo? Huyu hapa nabii mke anayeitwa Yezebeli naye anawafundisha watu. Na mafundisho yake yanawapotosha watumishi wa Mungu na kuwafanya wafanye uasherati. Sasa uasherati maana yake ni "kuabudu sanamu." Hiyo ndiyo maana yake ya kiroho. Ni muungano haramu. Muungano wa Ahabu na muungano wa Konstantino yote miwili ilikuwa haramu. Wote wawili walifanya uzinzi wa kiroho. Kila mzinzi ataishia kwenye ziwa la moto. Mungu alisema hivyo.

Haya basi, mafundisho ya Kanisa Katoliki (kanisa ni kiumbe cha kike, ni mwanamke) linakana Neno la Mungu. Papa ambaye ni Apolo mwenyewe kwa mtindo wa kisasa amewafundisha watu kujiunga na sanamu. Kanisa la Kirumi sasa limekuwa nabii wa kike wa uongo kwa watu kwa maana limeliondoa Neno la Mungu kutoka kwa watu na kutoa mawazo yake lenyewe juu ya jambo la msamaha wa dhambi, jambo linaloleta baraka za Mungu; na makasisi wamefikia kiwango cha kusema kwa mkazo kabisa kwamba wanayo mamlaka si katika maisha tu bali pia katika mauti. Wanafundisha wao wenyewe ya kwamba kuna pegatore, lakini huwezi kupata kitu hicho katika Neno. Wanafundisha ya kwamba maombi na misa na pesa zitakutoa kwenye toharani na kukuingiza mbinguni. Utaratibu wote ambao una msingi kwenye mafundisho yake ni wa uongo. Haupo katika msingi wa kweli wa ufunuo wa Mungu katika Neno Lake bali umekaa kwenye mchanga unaotembea unaozama wa uongo wake wa kishetani.

Kanisa lilienda moja kwa moja kutoka kwenye utaratibu likawa madhehebu kisha likayaendea mafundisho ya uongo. Hiyo ni kweli. Wakatoliki wa Kirumi hawaamini ya kwamba Mungu yuko katika Neno Lake. La bwana. Kama wangaliamini ingewabidi kutubu na kurudi, bali wao wanasema Mungu yuko katika kanisa Lake. Hilo lingeifanya Biblia kuwa ni historia ya Kanisa Katoliki. Sivyo ilivyo. Angalia kile walichofanya kwa ubatizo wa maji pekee. Waliuondoa kwenye kuwa Ubatizo wa Kikristo na kuufanya wa kipagani wa vyeo.

Hebu niwaambie juu ya tukio nililopata na kasisi Mkatoliki. Msichana fulani ambaye nilikuwa nimembatiza wakati mmoja aligeuka akawa Mkatoliki, kwa hiyo huyo kasisi alitaka kunihoji mimi kumhusu yeye. Akaniuliza alibatizwa kwa ubatizo wa namna gani. Nikamwambia nilimbatiza katika Ubatizo wa Kikristo ambao ndio tu wa aina yake uliokuweko nijuavyo mimi. Nilikuwa nimemzika majini katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Yule kasisi aliniambia ya kwamba wakati mmoja Kanisa Katoliki lilifanya hivyo. Papo hapo nikamwuliza ni lini Kanisa Katoliki lilifanya hivyo, kwa maana nimesoma historia zao nami sikuweza kupata alilosema. Akaniambia ya kwamba ulipatikana katika Biblia, na ya kwamba Yesu alikuwa ameunda utaratibu wa Kanisa Katoliki. Nilimwuliza kama alifikiri Petro alikuwa ndiye papa wa kwanza. Yeye akasema kwa msisitizo ya kwamba Petro alikuwa papa wa kwanza. Nikamwuliza kama ati misa ziliendeshwa katika Kilatini kusudi ihakikishwe kwamba hazina makosa na hazingebadilika kamwe. Yeye alisema hiyo ilikuwa ni kweli. Nikamwambia ya kwamba mimi nalifikiria wao walikuwa wametangatanga mbali sana na waliyokuwa nayo hapo mwanzo, nikamjulisha ya kwamba kama kweli Kanisa Katoliki liliamini Kitabu cha Matendo, basi mimi nilikuwa Mkatoliki wa mtindo wa kale. Akaniambia ya kwamba Biblia ilikuwa ni kumbukumbu ya Kanisa Katoliki na ya kwamba Mungu alikuwa katika kanisa. Sikukubaliana naye kwa kuwa Mungu yuko katika Neno Lake.

Mungu na aonekane kuwa amin na kila mtu mwongo. Kama ukiondoa ama kuongeza katika Kitabu hicho, Mungu ameahidi ya kwamba atawaongezea mapigo wale wanaoongeza na ataondoa sehemu yao kutoka kwenye Kitabu cha Uzima kama wakithubutu kuondoa kutoka kwake. Ufunuo 22:18, 19.

Hebu nionyeshe jinsi Kanisa Katoliki la Kirumi linavyoamini ya kwamba Mungu yuko katika kanisa badala ya kuwa katika Neno. Hapa pana maneno yaliyotolewa kwenye kitabu cha kumbukumbu habari za kila siku cha Papa Yohana wa 23. "Uzoefu wangu katika miaka hii mitatu kama Papa, tangu nilipokubali 'katika hofu na kutetemeka' utumishi huu katika utii halisi kwa mapenzi ya Bwana, niliyokabidhiwa kwa njia ya Baraza Takatifu la Makadinali lilipokutanika kisiri, unashuhudia msemo huu na ni sababu ya kuvutia na ya kunidumisha mimi kuwa mwaminifu kwake; kumtumaini Mungu kabisa, katika yale yote yanayohusu wakati uliopo, na utulivu mkamilifu kuhusu mambo ya usoni." Papa huyu anasema ya kwamba Mungu alinena kupitia kwenye kanisa akifunua mapenzi Yake. Ni uongo iliyoje. Mungu yuko katika Neno Lake na hunena kwa Neno akifunua mapenzi Yake. Yeye amesema pia ya kwamba aliweka tumaini kamilifu katika neno la wanadamu na hapo akalitii kwa utulivu. Linasikika ni zuri sana bali ni uongo sana. Kama tu ule upotovu katika Bustani ya Edeni.

Sasa hebu na tufungue hapa katika Ufu. 17 na tumwone mwanamke huyu, kanisa, ambaye anaishi kwa nabii za uongo na si kwa Neno la Mungu. Katika aya ya 1 Mungu anamwita kahaba mkuu. Kwa nini yeye ni kahaba? Kwa nini yeye ni kahaba? Kwa sababu yeye yuko katika ibada za sanamu. Yeye amewanasa watu katika jambo lile lile. Tiba ya kuabudu sanamu ni nini? Neno la Mungu. Kwa hiyo mwanamke huyu ni kahaba kwa sababu ameacha Neno. Huyo hapo ameketi juu ya maji mengi, ambayo yanamaanisha umati wa watu. Hili kweli halina budi kuwa ni lile kanisa la uongo kwa sababu kanisa la Mungu ni dogo_nao waionao ni wachache.

Tazama jinsi alivyo mbele za macho ya Mungu, haidhuru anaonekana ni mzuri sana vipi kwa watu na jinsi anavyosikika ni wa kifalsafa. Yeye ni mchafu na amelewa kwa uasherati wake. Sasa yeye alikuwa amelewa kwa damu ya wafia imani. Kama tu vile Yezebeli aliyewaua manabii na makuhani na

kuwaangamiza watu wa Mungu ambao hawangesujudu na kumwabudu Baali. Na hivyo ndivyo Kanisa Katoliki lilivyofanya hasa. Waliwaua wale ambao hawangejisalimisha kwa utawala wa Kipapa. Wale waliotaka Neno la Mungu badala ya maneno ya watu waliuawa, mara nyingi kwa njia za kikatili. Lakini kanisa hili ambalo lilishughulika na mauaji lilikuwa lenyewe limekufa na halikujua. Hamkuwemo na uhai ndani yake wala hamna ishara zilizopata kufuatana nalo.

**MUDA WA KUTUBU**

Ufunuo 2:21;

*"Nami nimempa muda ili atubu, wala hataki kuutubia uzinzi wake."*

Je! Mnajua ya kwamba kanisa hili lilikuwa kweli ni ovu kuliko Ahabu? Je! Unajua ya kwamba yeye alitubu kwa kitambo kidogo na kuenenda kwa unyenyekevu mbele za Mungu? Huwezi kusema jambo hilo kuhusu Kanisa Katoliki la Kirumi. La bwana. Halijatubu kamwe na kwa ukaidi limemwangamiza ye yote na wote waliojaribu kulisaidia kutubu. Hiyo ni historia. Halijatubu kamwe na kwa ukaidi limemwangamiza ye yote na wote waliojaribu kulisaidia kutubu. Yeye aliupa kila wakati watu wazuri sana wa Mungu nao wakafanya kila walichoweza kulirudisha kanisa kwa Mungu. Hakika Mungu alilipa nafasi na kulisaidia kutubu. Je! Lilipata kutubu na kuonyesha kwamba lilitubu kwa matunda yake? La bwana. Halijafanya hivyo na halitafanya hivyo. Limelewa. Limepoteza akili zake katika mambo ya kiroho.

Sasa msibabaike na kuanza kufikiri ya kwamba Kanisa la Kirumi limetubu kwa kuwaua watakatifu ati kwa sababu linajaribu kuungana na Waprotestanti kwa kufanya kanuni zake za imani zichukuane na Kanuni za Imani za Kiprotestanti. Hakuna hata wakati mmoja limewahi kuomba msamaha na kusema lilikuwa limekosea kwa mauaji yake ya umati. Wala halitatubu. Na haidhuru hata lionekane pole na jema namna gani katika wakati uu huu, hata hivyo bado litainuka lipate kuua, kwa maana kuua kunakaa kwenye moyo wake mwovu na usiotubu.

**HUKUMU IMETOLEWA DHIDI YA YULE KAHABA**

Ufunuo 2:22-23,

*"Tazama, nitamtupa juu ya kitanda, na hao wazinio pamoja naye, wapate dhiki kubwa wasipotubia matendo yao;*

*Nami nitawaua watoto wake kwa mauti; na makanisa yote watajua ya kuwa Mimi Ndiye achunguzaye viuno na mioyo. Nami nitampa kila mmoja wenu kwa kadiri ya matendo yake."*

Nini? Mwanamke huyu ana watoto? Naye ni kahaba? Kama hivyo ndivyo ilivyo ya kwamba yeye alipata watoto kwa ukahaba wake basi hana budi kuchomwa moto kama vile Neno lilivyosema. Hiyo ni kweli kabisa. Huo ndio mwisho wake kwa maana ataungua kwa moto. Mwisho wake ni ziwa la moto. Lakini simama na ufikirie juu ya watoto hawa kwa muda kidogo. Mwanamke ndiye yule ambaye watoto hutoka kwake. Ni dhahiri ya kwamba mwanamke huyu alikuwa na watoto waliotoka kwake lakini walifanya jambo lile lile alilolifanya. Nionyeshe kanisa moja lililopata kutoka kwenye madhehebu ambalo halikurudi ndani yake. Hakuna hata moja. Hakuna hata mmoja. Waluteri walitoka kisha wakaunda madhehebu wakarudi kule kule na leo hii wao ni kidole na pete katika pilikapilika za ekumeni. Wamethodisti walitoka wakaunda madhehebu moja kwa moja. Wapentekoste walikuja na wakaunda madhehebu moja kwa moja. Kutakuwako na mwingine atakayekuja, na Mungu asifiwe hawatarudi nyuma kwa sababu wanajua kweli. Kundi hilo litakuwa bibi-arusi wa siku ya mwisho.

Sasa ilisema hapa kwamba kahaba huyu alikuwa na watoto. Sasa walikuwa nani? Walikuwa ni binti, kwa kuwa walikuwa makanisa kama tu yeye alivyo. Sasa hapa kuna jambo la kuvutia sana. Yezebeli na Ahabu walikuwa na binti. Binti huyo aliolewa na Yehoramu mwana wa Yehoshafati na katika 2 Wafalme 8:16 inasema kwamba

*"Yehoramu alienda katika njia za baba mkwe wake."*

Yeye aliingia moja kwa moja katika ibada ya sanamu kwa ndoa hii. Aliiingiza Yuda inayomcha Mungu na inayomwabudu Mungu katika ibada ya sanamu. Hivyo ndivyo hasa haya makanisa washirika yote yalivyofanya, kama tu nilivyowaelezea. Wao wanaanza katika ile kweli kisha wanafunga ndoa na madhehebu na wanaacha Neno wachukue mapokeo, kanuni za imani nk. Sasa hebu nieleze jambo hili.

Katika Waebrania 13:7 inasema,

*"Watiini wao waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia Neno la Mungu."*

Neno ndilo linalotutawala, si wanadamu. Sasa mwanamume kama mume ndiye kichwa cha mwanamke. Anamtawala. Lakini kanisa ni mwanamke, pia, na mtawala wake ni Neno. Yesu ni Neno. Kama kanisa likikataa Neno na kukubali uongozi mwingine ni mzinzi. Sasa wewe nitajie kanisa moja ambalo halijaacha Neno na kuchukua mapokeo na kanuni za imani. Wote ni wazinzi—kama mama, kama binti.

Itakuwaje adhabu ya yule kahaba na watoto wake? Vema, itakuwa mara mbili. Kwanza Yeye alisema, "Nitamtupa kitandani." Kulingana na sehemu ya mwisho ya aya ya 22 itakuwa kitanda cha dhiki, ama ile dhiki kuu. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema katika Mathayo 25:1-13. Kulikuwako na wanawali kumi. Watano walikuwa wenye hekima na watano walikuwa wapumbavu. Wale watano wenye hekima walikuwa na mafuta (Roho Mtakatifu) lakini hao wengine watano hawakuwa nayo. Wakati kelele iliposikika, "Haya, Bwana Arusi yuaja," iliwabidi wale watano wapumbavu kukimbia wakitafuta mafuta huku wale watano wenye busara wakaenda kwenye arusi. Hao watano waliosalia nje waliachwa kwenye ile dhiki kuu. Hilo ndilo litakalowapata wote ambao hawatanyakuliwa. Hilo ndilo litakalompata yule kahaba na binti zake. Pili, inasema ya kwamba Yeye atawauwa kwa mauti ama kama tafsiri halisi inavyosema, "Na wauawe kwa mauti." Huu ni msemo wa ajabu. Tunaweza kusema, "mtu na auawe kwa kunyongwa, ama kwa umeme ama kwa njia fulani nyingine." Bali huu unasema, "Na wauawe kwa mauti." Mauti yenyewe ndiyo sababu ya kifo chao.

Sasa nawatakeni mwone jambo hili kwa dhahiri ili nichukue tena mfano wetu wa binti wa Yezebeli akiolewa katika nyumba ya Yuda na hapo akiiingiza moja kwa moja katika ibada za sanamu na kumfanya Mungu awapeleke Yuda mautini. Hivyo ndivyo Balaamu alivyofanya, pia. Kwa hiyo huyu hapa Yezebeli alikuwa na upagani wake. Upande ule yuko Yuda akimwabudu Mungu ipaswavyo na kuishi chini ya Neno. Kwa hiyo Yezebeli anamwoza bintiye kwa Yehoramu. Mara jambo hilo litukiapo, Yehoramu anawafanya watu kuwa waabudu sanamu. Mara hiyo ndoa ilipofungwa Yuda akawa amekufa. Mauti ya kiroho ikaingia. Mara tu kanisa la kwanza la Rumi lilipounda madhehebu, lilikufa. Mara Waluteri walipounda madhehebu, mauti iliingia nao wakafa. Wapentekoste walikuja mwisho nao wakaunda madhehebu. Roho akaondoka, hata ingawa wao hawaamini jambo hilo. Bali Roho aliondoka. Ndoa hiyo ilileta mauti. Ndipo nuru ya Umoja wa Uungu ikaja. Waliunda madhehebu nao wakafa pia. Ndipo baada ya moto wa Mungu kushuka kwenye Mto Ohio mnamo mwaka wa 1933 uamsho wa uponyaji ulienea ulimwenguni, bali haukuja kupitia dhehebu lolote. Mungu alitoka nje ya makundi ya Kipentekoste, nje ya madhehebu, na yale atakayofanya siku za usoni yatakuwa nje ya madhehebu, pia. Mungu hawezi kufanya kazi kupitia kwa wafu. Anaweza tu kufanya kazi kupitia kwa washiriki WALIO hai. Hao washiriki walio hai wako nje ya Babeli.

Kwa hiyo unaona, "Mauti" ama "Shirika" lilikuja, nalo kanisa likafa, ama kulifanya dhahiri zaidi mauti ikafanya makao mahali ambapo muda mfupi kabla yake ni UZIMA peke yake ulitawala. Kwa hiyo unaona, "Mauti" ama "Shirika" lilikuja, nalo kanisa likafa, ama kulifanya dhahiri zaidi mauti ikafanya makao mahali ambapo muda mfupi kabla yake ni UZIMA peke yake ulitawala na nabii mke Yezebeli. Sasa Hawa alipaswa kuchomwa moto pamoja na yule nyoka kwa ajili ya tendo lao baya. Lakini Adamu aliingilia kati, akamchukua haraka kwake ili apate kuokolewa. Bali wakati dini hii ya Kishetani itakapopitia katika kipindi chote kizima cha nyakati, hapatakuwa na mtu wa kuingilia kati, naye atachomwa moto pamoja na mwenye kulipotosha, kwa maana yule kahaba na watoto wake pamoja na mpinga Kristo na Shetani watatupwa wote katika ziwa la moto.

Papa hapa nitakuwa nikijitangulia na labda napaswa kuliacha jambo hili kwa ajili ya ujumbe juu ya wakati wa mwisho, bali linaonekana ni sawa tu kuliingiza sasa kwa maana linahusu kwa dhahiri sana madhehebu na kile kitakachotukia kupitia kwayo. Nami nataka kuwaonya.

Ufunuo 13:1-18,

> *"Kisha nikasimama juu ya mchanga wa bahari, na nikaona mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru.*
>
> *Na yule mnyama niliyemwona alikuwa kama chui, na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu, na kinywa chake kama cha simba; Yule joka akampa nguvu zake, na kiti chake cha enzi, na mamlaka kuu.*
>
> *Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona.*
>
> *Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?*
>
> *Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru; akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili.*
>
> *Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana Jina Lake, na maskani Yake, nao wakaao mbinguni.*
>
> *Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa.*
>
> *Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa*

*katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.*

*Mtu akiwa na sikio na asikie.*

*Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka; mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga; Hapa ndipo penye subira na imani ya watakatifu.*

*Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa mwana-kondoo, akanena kama joka.*

*Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake; naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona.*

*Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu.*

*Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi.*

*Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.*

*Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao;*

*Tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.*

*Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu; na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita."*

Sura hii inaonyesha nguvu za Kanisa Katoliki la Kirumi na yale litakalofanya kwa kupitia kwenye shirika. Kumbuka huu ni mzabibu wa uongo. Acha utaje Jina la Bwana, unafanya hivyo kwa uongo tu. Uongozi wake si wa Bwana bali wa Shetani. Hatimaye unaishia ambapo unatambulishwa na mnyama kabisa. Yule kahaba akiketi juu ya mnyama mwekundu sana inaonyesha kwa dhahiri nguvu zake ni za mungu anayetumia nguvu (Shetani) na si Mungu wetu, Bwana Yesu Kristo.

Katika aya ya 17 inaonyesha kwa mkazo ya kwamba yeye atatwaa mamlaka kabisa juu ya uchumi wa dunia, kwa maana hakuna mtu awezaye kununua wala kuuza bila yeye. Hili linathibitishwa katika Ufu. 18:9-17 ambapo anaonyeshwa akijihusisha na wafalme, watawala, wafanyi biashara, ambao wote wana uhusiano na Rumi na biashara.

Katika Ufu. 13:14, tunapata kujua ya kwamba yule mnyama anaeneza ushawishi wake kwa kupitia sanamu aliyojengewa. Sanamu iliyojengwa ni baraza la ekumeni la dunia nzima, ambamo makanisa yote yaliyounda madhehebu yatakutanika pamoja na Wakatoliki wa Kirumi (hata sasa hivi wanafanya hivyo.) Inawezekana kabisa muungano huu utakuja kusitisha nguvu za ukomunisti. Lakini kwa sababu ukomunisti kama vile Nebukadreza umeinuliwa ili kuuunguza mwili wa yule kahaba, Rumi itashindwa na kuangamizwa. Angalia kwamba kila mahali kanisa la Kirumi lilipoenda, ukomunisti ulifuata. Haina budi kuwa hivyo. Na hebu niwaonye sasa, msifikiri ukomunisti ndio adui yenu pekee. La bwana. Ni Kanisa Katoliki pia, na hata na zaidi.

Sasa hebu na tusome Ufunuo 13:1-4, na tulinganishe hili na Ufunuo 12:1-5. Ufunuo 13:1-4,

*"Kisha nikasimama juu ya mchanga wa bahari, nikaona mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi, na juu ya vichwa vyake jina la makufuru.*

*Na yule mnyama niliyemwona alikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu, na kinywa chake kama kinywa cha simba; yule joka akampa nguvu zake, na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi.*

*Nami nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona; dunia yote ikamstaajabia mnyama yule.*

*Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? tena ni nani awezaye kufanya vita naye?"*

Ufunuo 12:1-5,

*"Na ishara kuu ikatokea mbinguni; Mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili;*

*Naye alikuwa ana mimba, akilia, hali ana utungu na kuumwa katika kuzaa.*

*Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba.*

*Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake.*

*Naye akazaa mtoto mwanamume, yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma; na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwenye kiti Chake cha enzi."*

Shetani na dini yake ya Kishetani wamo katika wanyama hawa wawili. Katika Ufu. 14, yule mnyama aliyetiwa jeraha la mauti lakini akaishi tena ni milki ya kipagani ya Rumi ambayo iliangushwa na mashambulizi ya washenzi na hapo ikapoteza nguvu zake za kitaifa. Bali ilizipata tena kupitia Rumi ya papa. Mnaona jambo hilo? Taifa lile lililotawala kwa kuwavunjavunja wote na ambalo lilifanyika dola yenye nguvu sana iliyopata kujulikana, hatimaye lilitiwa jeraha la mauti. Nguvu zake za kitaifa kama kutawala kwa majeshi nk. zilikwisha. Bali chini ya Konstantino liliishi tena, kwa maana Rumi ya papa imepenyeza kila mahali duniani, na nguvu zake hazina kikomo. Inawatumia wafalme na wafanyi biashara na katika nguvu zake hatari za kidini na za kifedha inatawala kama mungu mke wa wakati huu wa sasa. Hiyo pia ndiyo yule joka aliyesimama apate kumla mtoto mwanamume. Herode alijaribu kumwua Bwana Yesu na akashindwa. Baadaye Yesu alisulubiwa na askari wa Kirumi, lakini sasa amenyakuliwa kwenye kiti cha enzi.

Sasa pamoja na yale niliyosema hivi karibuni, kumbukeni lile ono la Danieli. Sehemu ya mwisho ya ile sanamu, ile mamlaka ya mwisho ya ulimwengu ilikuwa miguuni. Hiyo ilikuwa chuma na udongo. Ona ile chuma ni Dola ya Kirumi. Lakini sasa si chuma tena kigumu. Udongo umechanganywa ndani yake. Hata hivho ipo pale na inatawala shughuli za dunia katika mataifa ya kidemokrasia na yale yaliyozidi katika kutawala kwa mabavu. Kanisa la Kirumi liko katika kila taifa. Limechanganyikana na hayo yote.

Hebu niwape kitu fulani kidogo juu ya chuma na udongo. Mnakumbuka wakati Khrushchev alipogonga meza kwa kiatu chake kwenye U.M.? Vema, kulikuweko na mataifa matano ya mashariki hapo na matano ya magharibi. Khrushchev alizungumza kwa ajili ya Mashariki na Rais Eisenhower kwa Magharibi. Katika Kirusi, Khrushchev ni udongo na Eisenhower maana yake ni chuma. Viongozi wawili wakuu wa ulimwengu, vidole viwili vikubwa vya miguu ya chuma na udongo, vilikuwa pamoja. Sisi tuko katika mwisho wa yote.

Katika aya ya 4 inauliza,

*"Ni nani awezaye kufanya vita na yule mnyama?"*

Naam kwa sasa kuna majina makubwa ulimwenguni. Kuna baadhi ya mataifa yenye nguvu, bali sasa hivi Rumi ndiyo inayotawala. Papa yuko kwenye kiti cha dereva. Na nguvu zake zitaongezeka. Hakuna mtu anayeweza kupigana naye.

Mstari wa 6,

*"Akafunua kinywa chake amtukane Mungu."*

(Wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa, wenye mfano wa utauwa huku wakikana nguvu zake.) Yeye alilitukana Jina la Mungu_akilibadilisha Jina hilo kuwa vyeo na kukataa kufanya vinginevyo.

Mstari wa 7,

*"Tena akapewa kufanya vita na watakatifu."*

Mateso_mauti kwa mwamini wa kweli na yote katika Jina la Bwana kusudi Jina la Mungu litukanwe, kama ilivyo kule Urusi, kwa sababu ya yale dini ya Katoliki ilivyofanya kule.

Mstari wa 8,

*"Na watu wote wakaao juu ya nchi (wote ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia) watamsujudu."*

Asante Mungu kondoo hawatamsujudu. Kila mtu atadanganywa isipokuwa wale walio wateule. Lakini wao hawatadanganywa. Kwa kuwa wanaisikia sauti ya Mchungaji nao wanamfuata.

Sasa basi, angalieni hili, yale tumekuwa tukijaribu kuwaonyesha. Hii mbegu ya mauti iliyoanza katika wakati wa kwanza_hii mbegu ya kimadhehebu, hatimaye imekua ikawa mti ambamo kila ndege mchafu anakaa. Mbali na madai yake kuwa yeye ni mpaji wa uzima, yeye ni mpaji wa mauti. Tunda lake ni MAUTI. Wale wanaomshiriki wamekufa. Taratibu hii kuu ya kanisa la ulimwengu ambayo huupumbaza ulimwengu ya kwamba ndani yake mna wokovu wa kimwili na wa kiroho huwadanganya na kuwaangamiza watu wengi mno. Lakini yeye si mauti tu katika mwili, bali kiumbe hiki cha mzoga huu uliokufa wenyewe utauawa kwa mauti ambayo ni ziwa la moto. Loo! laiti watu wangalijua mwisho wao utakakuwa ni nini wakibaki ndani yake. "Tokeni kwake, kwa nini mfe?"

**ONYO LA MWISHO**

Ufunuo 2:23.

> *"Nami nitawaua watoto wake kwa mauti. Na makanisa yote watajua ya kuwa Mimi Ndiye achunguzaye viuno na mioyo. Nami nitampa kila mmoja wenu kwa kadiri ya matendo yake."*

Mungu huangalia moyo. Hilo halijabadilika kamwe. Wala halitabadilika kamwe. Hapa, kama vile katika nyakati zote kuna makundi mawili, yote yakidai ufunuo wao kutoka kwa Mungu na uhusiano wao na Mungu.

> *"Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye muhuri hii, Bwana awajua walio Wake."*

II Timotheo 2:19.

> *"Bwana huchunguza viuno."*

*Neno 'tafuta' linamaanisha 'kufuatilia' ama 'andama.'* Mungu hufuatilia mawazo yetu (viuno); Yeye anajua kilicho mioyoni mwetu. Yeye huziona kazi zetu ambazo ni madhihirisho dhahiri ya yale yaliyo ndani yetu. Ni kutoka moyoni ambamo hutoka aidha haki ama maovu. Madhumuni yetu, makusudi yetu_yote yanajulikana Kwake kwa kuwa Yeye huchunguza kila tendo. Na kila tendo, kila neno litaletwa hukumuni wakati hesabu ya maisha yetu itakapotolewa. Hapakuwepo na kumcha Mungu mbele ya ule mzabibu wa uongo na wao watalipia kwa uchungu. Hebu wote wanaolitaja Jina Lake, waishi inavyowapasa watakatifu. Tunaweza kuwadanganya watu lakini hatuwezi kumdanganya Bwana.

**AHADI KATIKA SIKU ZILE ZA GIZA**

Ufunuo 2:24-25.

> *"Lakini nawaambia ninyi, na wengine mlioko Thiatira, wo wote wasio na mafundisho hayo, wasiozijua fumbo za Shetani, kama vile wasemavyo, Sitaweka juu yenu mzigo mwingine.*
>
> *Ila mlicho nacho kishikeni sana, hata nitakapokuja.*"

Sasa kabla hatujaingilia ile ahadi hebu nionyeshe tena ya kwamba kanisa kama lilivyonenwa na Roho katika kitabu hiki lina mizabibu miwili ambayo inaunda kanisa hili kwa matawi yake yaliyosukana.

> *"Lakini nawaambia ninyi, na hao wengine wote walioko Thiatira wasio na mafundisho haya."*

Hilo hapo. Yeye anazungumza na makundi hayo mawili. Mmoja ana fundisho, mwingine hana. Hayo hapo, wametawanyika kila mahali katika mataifa huku fundisho la kila mmoja wao likipingana na la mwingine. Moja ni la Mungu, likijua fumbo zake, hilo lingine ni la Shetani, likijua fumbo za Shetani.

*"Sitaweka juu yenu mzigo mwingine."*

Neno jingine badala ya mzigo ni uzito ama dhiki. Dhiki ya zile Zama za Giza ilikuwa aidha ukubali, ama uvunjiliwe mbali. Sujudu la sivyo ufe. Ilikuwa ni lile baraza kuu la kuhukumu waamini, nguvu za dola zikiunga mkono ibada za Kishetani. Unda madhehebu la sivyo utalipa kwa uhai wako. Kila wakati ulikuwa na dhiki zake Kwa mfano mzigo mkubwa wa wakati wa mwisho ni matatizo ya utajiri, kuishi maisha ya raha na wasiwasi wa mawazo katika wakati wenye mambo chungu mbovu ambamo inaonekana ni vigumu kwetu kuishi ndani yake. Wakati huu wa nne ulionekana kama kwamba ulikuwa na mzigo wa wazi wazi. Ulikuwa ni wa kuasi Rumi, kusimama imara na Neno hata kufa.

*"Wasiozijua fumbo za Shetani."*

Inaonekana ya kwamba aya hii imeachwa na wafafanuzi kwa kuwa wao hawakuweza kujua ni fundisho gani ama ni ujuzi gani uliomaanishwa na kifungu hiki. Kwa kweli ni rahisi kujua unamaanisha nini. Hebu kwanza tujue fumbo la Mungu ni kitu gani, na kinyume chake ndicho kitakachokuwa fumbo la Shetani.

Katika Waefeso 3:16.

*"Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho Wake, katika utu wa ndani;*

*Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo,*

*Ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina;*

*Na kuujua upendo Wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu."*

Sasa kulingana na aya hizi, wakati mtu anapopata ujuzi wa kina cha Mungu katika maisha yake, ni tukio halisi la kibinafsi la Roho wa Mungu akiishi ndani yake, na nia yake inaangazwa na hekima na maarifa ya Mungu kwa kupitia Neno. Lakini kina cha Shetani kitakuwa kwamba yeye atajaribu kuangamiza jambo hilo. Yeye daima atajaribu kufanya badiliko la ukweli huu wa Mungu. Atafanyaje jambo hilo? Ataondoa maarifa ya ukweli wa Mungu_kuliangamiza Neno kwa kuweka lake mwenyewe, "Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu?" Hapo basi yeye atabadilisha utu wa Kristo katika roho zetu. Atabadilisha, kama vile alivyowafanya Israeli kufanya jambo lile lile; kwa mwanadamu akitawala kama mfalme badala ya Mungu. Tukio la kuzaliwa mara ya pili litakataliwa kwa kupenda kujiunga na kanisa. Fumbo za Shetani zilikuwa zimeingizwa ndani katika wakati huo. Na tunda la fumbo hilo la Shetani ambalo ni uongo, mauaji na uharibifu wa kutisha yalitokana na jambo hilo.

**THAWABU**

Ufunuo 2:26- 29.

*"Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo Yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa,*

*Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, kama vyombo vya mfinyanzi vipondwavyo, kama Mimi Nami nilivyopokea kwa Baba Yangu.*

*Nami nitampa ile nyota ya asubuhi.*

*Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.*

*"Yeye ashindaye na kuyatunza matendo yangu hata mwisho."*

*Ni dhahiri sana kutokana na matamshi ya Roho juu ya kazi ya kwamba Bwana anajaribu kuwafanya walio Wake kuona maoni Yake ya kazi za haki.* Anataja kazi mara nne. Na sasa Yeye anasema, ya kwamba yeye anayeendelea kutenda kazi Zake kwa uaminifu hata mwisho atapewa mamlaka juu ya mataifa, naye atakuwa kiongozi mwenye nguvu, hodari, shupavu ambaye anaweza kukabiliana vizuri sana na hali yo yote, kwamba hata adui aliye mbaya sana atavunjwa kama kukiweko na haja. Dhihirisho Lake la kutawala kwa mamlaka litakuwa kama lile lile la Mwanawe Hili ni la kushangaza sana.

Lakini hebu na tuangalie ahadi hii katika nuru ya wakati huo. Rumi yenye nguvu ikiungwa mkono na serikali, ikiwatumia wafalme na majeshi na wabunge, inavunja-vunja na kusaga yote yaliyo mbele zake. Imewaua mamilioni na inaona njaa ya kuwaua mamilioni wengine ambao hawatamsujudu. Inawatawadha wafalme na kuwashusha bila kuvumilia wakati wo wote awezapo. Naam, kuingilia kwake kati kwa kweli kumeyafanya mataifa kuanguka kwa maana amepania kuwaangamiza wateule wa Mungu. Kazi zake ni kazi za ibilisi, kwa kuwa huua na kudanganya kama ibilisi alivyofanya. Lakini siku inakuja ambapo Bwana atasema, "Waleteni hawa adui Zangu mbele Yangu mkawaue." Ndipo wenye haki watakapokuwa na Bwana wao wakati hasira Yake yenye haki itakaposhuka juu ya wanaokufuru. Wale wenye haki watakapokuja Naye katika utukufu, watawaangamiza hao walioiharibu nchi na kuwaangamiza watakatifu wa Mungu. Huu ulikuwa ni wakati wa kugeuza hilo shavu lingine, wa dhiki mbaya sana; lakini siku inakuja wakati kweli itashinda na ni nani atakayesimama katika moto wake na awe salama? Ni wale tu waliokombolewa na Bwana.

*"Nami nitampa ile nyota ya asubuhi."*

Kulingana na Ufunuo 22:16, na II Petro 1:19, Yesu ndiye Nyota ya Asubuhi.

*"Mimi Ndimi niliye Shina na Mzao wa Daudi, ile nyota yenye kung'aa ya asubuhi."*

*"Mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu."*

Roho kwa hiyo basi, anawapa wateule wa zile Zama za Giza ahadi kuhusiana na Yeye Mwenyewe na halafu pia katika nyakati zijazo.

Kama tulivyokwisha kusema, Yesu anajitambulisha Mwenyewe na wajumbe wa kila wakati. Wanapokea kutoka Kwake ufunuo juu ya Neno kwa ajili ya kila kipindi. Ufunuo huu wa Neno huleta wateule wa Mungu kutoka ulimwenguni na kuwa katika umoja kamili na Yesu Kristo. Wajumbe hawa wanaitwa nyota kwa sababu wao wanawaka kwa nuru ya kuazima ama nuru wanayoitoa na wao ya Mwana, yaani Yesu. Wao wanaitwa nyota pia kwa sababu wao ni 'wabebaji wa nuru' usiku. Kwa hiyo katika giza la dhambi, wanaleta nuru ya Mungu kwa watu Wake.

Hizi ndizo zile Zama za Giza. Ni giza hasa kwa sababu Neno la Bwana karibu lote limefichwa kabisa kwa watu. Maarifa ya Yeye Aliye Juu karibu yamekoma. Kifo kimepiga idadi kubwa sana ya waamini mpaka makundi yao yamepunguka. Mambo ya Mungu yako katika hali ya kufifia sana mpaka kufikia wakati huu, na ilionekana ya kwamba hakika Shetani angewashinda watu wa Mungu.

Kama watu walipata kuhitaji ahadi inayoshikilia nchi ambamo hakuna usiku, ilikuwa ni wale watu wa Nyakati za Giza. Na hiyo ndiyo sababu Roho anawaahidi ile nyota ya asubuhi. Yeye anawaambia hivyo ya kwamba ile Nyota Kuu, yaani Yesu, Ambaye anaishi katika Nuru ambayo hakuna mtu awezaye kuikaribia, atawaangazia katika ufalme ujao kwa uwepo Wake Mwenyewe. Yeye hatakuwa akitumia zile nyota (wajumbe) kutoa nuru gizani tena. Itakuwa ni Yesu, Mwenyewe, akinena nao uso kwa uso anaposhiriki ufalme Wake pamoja nao.

Nyota ya asubuhi ndiyo inayoonekana wakati nuru ya jua inapoanza kuangaza. Wakati Jua letu, (Yesu) atakapokuja, hakutakuwa na haja tena ya wajumbe; Yeye atatuletea ujumbe Wake wa Mwenyewe wa furaha; na anapoutawala ufalme Wake, nasi tunaishi katika uwepo Wake, nuru ya Neno itazidi kung'aa zaidi na zaidi katika siku yetu kamilifu.

Ni kitu gani kingine tungeweza kutamani zaidi ya Yesu Mwenyewe? Je, Yeye si ni kila kitu, hata kila Kitu kilicho Kikamilifu?

Yeye aliye na sikio, na alisikie hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Amina. Hata hivyo, Bwana Mungu, kwa Roho Wako, jalia tusikie kweli Yako.

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7